



SUZA

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR



www.suza.ac.tz

Kichocheo cha Mabadiliko ya Jamii

KIGODA CHA T CHA SHEIKH ABED A



Salamu kutoka kwa Makamu Mkuu wa Chuo



Wapendwa wasomaji wetu, tunafuraha kukuleteeni toleo jingine la jarida letu la robo mwaka lililojaa habari na taarifa mbalimbali kuhusu matukio ya hivi karibuni kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Toleo hili linamulika mafanikio tuliyoyapata katika kufikia malengo yetu.

Kama tunavyofahamu, elimu ya juu imepewa umuhimu mkubwa katika nchi yetu. Kwa hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya juhudi kubwa za kuendeleza sekta hii.

Tangu awamu ya kwanza ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, viongozi wote wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa

elimu katika mchakato wa maendeleo ya Zanzibar. Upatikanaji wa maendeleo endelevu unategemea sana mazingira mazuri ya elimu.

Hii ndiyo sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliazimia kuanzisha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa kutungwa kwa Sheria ya Baraza la Wawakilishi Na. 8 ya mwaka 1999.

Leo tunahesabu miaka 23 ya shughuli rasmi za Chuo Kikuu. Tangu mwaka 2001, SUZA imepiga hatua kubwa katika ukuzaji elimu kwenye nyanja mbalimbali, ambapo sasa wahitimu wake wanachangia maendeleo ya nchi.

Katika kuitikia wito wa serikali wa kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar, SUZA imedhamiria kutimiza lengo hilo kwa kutoa elimu bora inayokidhi mahitaji ya sasa ya soko na ustawi wa watu.

Hii inaonesha njia na mipango mbalimbali inayotumika kuleta

upatikanaji wa elimu sahihi.

Lengo kuu la jarida hili ni kuwajulisha wasomaji wetu na umma kwa ujumla kuhusu baadhi ya matukio ya hivi karibuni yaliyotokea SUZA.

Dhamira yetu ni kutoa taarifa kwa uwazi juu ya matukio yote yanayotokea SUZA kwa manufaa ya Chuo Kikuu na taifa kwa ujumla.

Kwa hivyo, nawasihi nyote muendeleo kusoma toleo hili na lile litakalotolewa siku za usoni ili muendeleo kuwa na taarifa na tusipitwe na matukio yanayotokea upande wetu.

Karibuni nyote kupata taarifakamilizamatukioyetu.

Ahsanteni,

Prof. Moh'd Makame Haji
Makamu Mkuu wa Chuo



Dk. Hussein ahimiza kufanywa tafiti

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye pia ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Dk. Hussein Mwinyi, ametoa wito kwa jamii ya SUZA kuzingatia zaidi utafiti kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Akizindua Kigoda cha Taaluma cha Sheikh Abeid Amani Karume katika Kampasi ya SUZA, Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja, Dk. Mwinyi alieleza kuwa matokeo ya tafiti hizo yatasaidia watunga sera kupanga mipango ya maendeleo kwa ufanisi.

Dk. Mwinyi aliongeza kuwa tafiti pia zitasaidia kutambua changamoto na fursa zilizopo katika sekta mbalimbali, na kwamba watumiaji wa tafiti hizo ni pamoja na wadau wa maendeleo na Serikali. Alisisitiza umuhimu wa kufanya tafiti na kazi nyingine za kitaaluma kupitia Kigoda cha Karume ili kustawisha taaluma na kuleta mchango katika jamii.

“Mtakapofanya hivyo mtakuwa mmekitendea haki Kigoda hiki na kumuenzi kwa vitendo Mzee wetu Marehemu Abeid Amani Karume,” alisisitiza Dk. Mwinyi.

Kigoda cha Taaluma cha Sheikh Abeid Amani Karume kina malengo ya kuhifadhi, kuenzi, na kuendeleza fikra za Sheikh Abeid Amani Karume katika kuleta ukombozi na maendeleo ya Zanzibar, kufanya SUZA kuwa mahali pa majadiliano, kuendeleza ushirikiano ndani na nje ya Afrika, na kukuza uwezo wa vijana na wasomi wanaochipukia kwa kuwashirikisha katika tafiti, makongamano, mikutano, na mijadala ya Kigoda.

Balozi wa Kigoda hicho, Dkt. Amani Abeid Karume, ambaye ni Rais mstaafu wa Awamu ya Sita wa Zanzibar, alipongeza hatua hii na kueleza kuwa kuanzishwa kwa Kigoda ni kufungua ukurasa mpya wa historia. Alisema kuwa hii itakuwa ni chachu ya ukombozi na

maendeleo ya nchi. Aliwataka vijana kuenzi mawazo na fikra za muasisi huyo kwa kuwa wadadisi kwa watu waliowazidi umri na kuzipitia nyaraka muhimu za kihistoria iliziweze kuwasaidia. “Waulizeni hao asilimia sita ya watu waliobakia ambao walizaliwa kabla ya Mapinduzi ya 1964, watakwambieni wanajua mambo ambayo nyinyi hamyajui,” alishauri.

Dkt. Karume alisema ni muhimu viongozi kuenzi fikra za Mapinduzi kwa kudumisha umoja, kupinga ubaguzi wa aina yoyote, na kutoa elimu kwa usawa bila kujali sura, rangi, au eneo la kijografia. Alifahamisha kuwa haya ndio malengo ya Mapinduzi yaliyoongozwa na Marehemu Karume na wenzake, hivyo ni lazima yaendelezwe katika kufanikisha lengo la kuanzishwa kwa Kigoda.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa SUZA Prof. Moh’d Makame Haji, alisema lengo la kuanzishwa kwa Kigoda hicho ni kuhifadhi, kuenzi, na kuendeleza mawazo na fikra za Sheikh Abeid Amani Karume katika kuleta ukombozi na maendeleo. Alisema Kigoda kitaandaa mijadala itakayolenga kutafuta ufumbuzi wa changamoto kwenye nyanja za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, na kisayansi ili kuifanya SUZA kuwa kichocheo cha mabadiliko ya jamii. Nae Mwenyekiti mteule wa Kigoda,

Prof. Egnald Mihanjo, alisemakuna kazi kubwa ya kuwajengea hamaşa vijana kwani hawajui ukoloni wala uhuru. Aliongeza kuwa hoja nyingi zinazozungumzwa na vijana hazina uzalendo, hazikuzi Mapinduzi wala uchumi. “Ni vyema kuangalia mikakati na mbinu za Mzee Karume na kuzitumia ili kujenga nchi kwa kutumia falsafa zake,” alisema.

Akichangia mijadala huo, Rais mstaafu wa Awamu ya Nne wa

Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alisema Kigoda ni kitu cha heshima kinacholenga kuendeleza tafiti na taaluma. Alisema SUZA imekuja na uamuzi sahihi kuanzisha Kigoda hiki ambacho kitajikita katika ukombozi na maendeleo ya Afrika.

Aliendelea kueleza kuwa Vigoda hutoa fursa ya kuimarisha na kuchochoea maendeleo ya fani maalum huko vikitoa fursa ya kukuza ushirikiano na kuimarisha sera ya umataifishaji wa Vyuo Vikuu. Alishangazwa na hulka iliyopo ya vyuo vikuu katika zama hizi kukosa mchanganyiko wa wanataaluma kutoka mataifa mbalimbali tofauti na ilivyokuwa zamani wakati wao wanasoma.

Alisisitiza umuhimu wa utafiti kwa maendeleo na kutoa wito kwa SUZA kuzalisha vigoda vingine kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kina vigoda kadhaa vikiwemo Kigoda cha Maendeleo ya Mwalimu Nyerere na Kigoda cha Mazingira.

Kwa upande wake Rais mstaafu wa Awamu ya Saba Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein alisema Kigoda kina jukumu kubwa la kuyatunza Mapinduzi na kudumisha Muungano. Alisisitiza kuwa ni lazima kuyakumbuka Mapinduzi na ni haki na wajibu kufanya hivyo ili kuipiga vita ubaguzi. Dkt. Shein pia alieleza umuhimu wa utafiti unaochambua mustakbali wa taifa kwa kuoanisha na dira, fikra na maono ya marehemu Sheikh Karume. Akichangia mijadala huo,

Mwanasiasa mkongwe nchini Bwana Stephen Wasira alieleza historia ya Zanzibar na namna ukombozi ulivyopatikana. Alisema Zanzibar ilikuwa imegubikwa na ubaguzi ambao Marehemu Karume alipingana nao kuhakikisha anaondoa matabaka yaliyokuwepo.



Kiswahili chaipaisha SUZA kimataifa

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Naiibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taaluma ya Asia-Magharibi na Afrika ya China Prof. Wang Xiaoming amesema kuwa ameridhishwa na uhusiano uliopo baina ya taasisi anayoiongoza na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA). Amesema SUZA imekuwa mashuhuri kutokana na mipango yake madhubuti ya uendeshaji na uzalishaji wataalamu wa ndani na nje ya nchi. Prof. Wang ameyaeleza hayo katika kikao cha pamoja kilichofanyika Kampasi ya Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja baina ya SUZA na taasisi anayoiongoza kilichowashirikisha pia wanataaluma kutoka SUZA na ujumbe kutoka taasisi hiyo. Amefahamisha kuwa SUZA inatambulika kutokana na wanafunzi wengi kupitia hapa kujifunza lugha ya Kiswahili na taaluma nyengine. Aliongeza kuwa mwaka 2013 Vyuo hivyo vilisaini mkataba wa makubaliano ambapo matarajio yao ni kuendeleza uhusiano mwema uliopo na kushirikiana katika nyanja mbalimbali za kitaaluma. Alibainisha kuwa kati ya mwaka 2015 hadi 2017 walifanikiwakuleta wanafunzi saba (7) SUZA kujifunza lugha ya Kiswahili. Aidha, kiongozi huyo aliongeza kuwa kuanzia mwaka 1961 walianza kufundisha Lugha ya Kiswahili ikiwa ni taasisi ya mwanzo nchini humo kufundisha Kiswahili. Alieleza kuwa hivi sasa kuna lugha 20 za Kiafrika zinazofundishwa ambapo lugha nyengine zaidi ya 100 za nchi mbalimbali pia zinafundishwa. “Tuna wanafunzi zaidi ya 1,000 waliopata mafunzo ambao wanashiriki katika kazi zinazohusiana na lugha za kimataifa, wamezalisha pia Mabalazi wa Umoja wa Wanafunzi 5,000 katika nyanja ya lugha”, Prof. Wang alisema. Alifahamisha kuwa Tanzania na China ni marafiki wa kweli tangu miaka ya 1950 ambapo wanapofikiria nchi za Afrika, kwanza wanaingalia Tanzania ikiwemo Zanzibar. Prof. Wang ambaye ni mkuu wa msafara wa wajumbe sita (6) alioongozana nao alitoa fursa kwa

SUZA kujadiliana na wanafunzi wa skuli zao kuhusu ushirikiano wa kiuchumi baina ya China na Tanzania pia amewakaribisha wanafunzi wanaopenda kujifunza lugha ya Kichina kutembelea nchi yao na wanafunzi wa China kuja Zanzibar kujifunza Kiswahili.

Naye Naiibu Makamu Mkuu wa SUZA anayeshughulikia Mipango, Fedha na Utawala, Dkt. Hashim Hamza Chande alisema SUZA imekuwa ikipata mafanikio makubwa kutokana na uhusiano uliopo kati ya Zanzibar na China ambao unahitaji kudumishwa zaidi kwa kuangalia maeneo mengine ya kitaaluma. “Tuna madarasa la Kichina (Confucious Classes) na tuna wazungumzaji mahiri wa lugha

hii, tunashukuru kupata fursa ya kuzungumza na wanafunzi wenu, hali itakayochangia kutanua wigo wa uhusiano uliopo”, alikumbusha.

Mapema, Bi. Shani Khalfan Suleiman, Mkuu wa Idara ya Kiswahili kwa Wageni, alisema wamekuwa wakiwasiliana na wataalamu wenzao wa China ili kuimarisha programu za ufundishaji wa lugha nyengine.

Katika kikao, hicho wajumbe walikubaliana kuupitia tena mkataba wa makubaliano pamoja na kuziba pengo la kutokuwepo walimu wazawa wa Kitanzania wanaofundisha lugha ya Kiswahili nchini China ambapo walimu wengine kutoka mataifa yasiyozungumza Kiswahili kama lugha yao ya kwanza wakiitumia vyema fursa hiyo.

Watendaji, wanafunzi wafundwa elimu ya mafao ZSSF

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Wafanyakazi na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) wamepatiwa elimu kuhusiana na fidia kwa wafanyakazi katika sehemu za kazi ili kutambua haki zao na kuzidai kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.

Mafunzo hayo yametolewa na maafisa kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) tarehe 15 Mei, 2024.

Katika mafunzo hayo, yaliyofanyika katika Kampasi ya Tunguu WanaSUZA walifunzwa aina sita (6) za mafao ikiwa ni pamoja na mafao ya kila mwezi kwa kila mfanyakazi mwanachama wa Mfuko wa ZSSF, mfanyakazi anayeumwa na hawezi kurudi kazini, fao la maradhi, upotevu wa ajira, fao la uzazi kwa akinamama wanaojifungua na fao la fidia kazini.

Akitoa mafunzo hayo, Ofisa anayeshughulikia fidia kwa

wafanyakazi katika sehemu za kazi kutoka Mfuko wa ZSSF, Bwana Masoud Mrisho alisema utoaji wa huduma za Mfuko umeimarika na kwamba kwa sasa fidia ndizo zinazosubiri mteja kupatiwa badala ya kusubiri muda mrefu kama ilivyokuwa hapo zamani.

Alifahamisha kuwa jambo la msingi ni lazima mteja awe amekamilisha vielelezo vinavyostahiki kuwasilishwa ikiwa ni pamoja na kuwa mwanachama, awe anachangiwa kwenye mfuko na awe amepata ajali.

Akizungumzia kuhusu upatikanaji wa mafao hayo, aliwashauri wafanyakazi endapo watapata maafa katika sehemu za kazi ni vyema wakawa wakweli na kuwa na vielelezo vinavyostahiki.

Katika mafunzo hayo wafanyakazi walielezea kuridhishwa kwao kwani walipata fursa ya kuuliza maswali kadhaa waliyokuwa nayo kuhusiana na mfuko.





SUZA yazidi kupanua wigo ushirikiano wa kielimu

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Makamu wa Rais wa Chuo Kikuu cha Mawasiliano cha Zhejiang (Communication University of Zhenjiang - CUZ) Profesa Yao Zheng, ameahidi kuendeleza ushirikiano uliopona Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kupitia utaratibu wa mkataba maalum wa makubaliano (MoU) wa kubadilishana walimu na wanafunzi, utafiti na maeneo mengine ya taaluma ya habari na mawasiliano kwa maslahi ya China na Zanzibar. Akimkaribisha Mkuu wa Idara ya mafunzo ya Mawasiliano na Habari wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Dkt. Khamis Juma Abdalla aliyetembelea Chuo hicho, Profesa Zheng alisema kuwa ushirikiano wa China na Afrika una mizizi mirefu na

unahitaji kudumishwa. Katika ushirikiano huo, kwa upande wa Zanzibar Chuo hicho kimekuwa kikitekeleza ushirikiano kupitia mradi maalum wa udhamini wa masomo ya uandishi wa habari chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar. Katika mradi huo, wanafunzi kutoka Zanzibar wamekuwa wakinufaika kwa kupata nafasi za masomo ya kada ya habari, jambo linalokuza vipaji na taaluma katika utangazaji, sanaa na ubunifu wa uandishi wa habari. Kwa upande wake, Dkt. Abdalla alitoa shukurani zake kwa ukaribisho na kusema kuwa kuwepo kwa ushirikiano huo kutasaidia kufikia azma ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kupitia Idara ya Mafunzo ya Habari na Mawasiliano ya kukuza vipaji vya vijana kuwa waandishi wa habari wenye dira

na uwezo wa kiubunifu kimataifa.

Aidha, aliongeza kuwa ushirikiano huo utakuza maendeleo ya kitaaluma kupitia tafiti za kisayansi juu ya mawasiliano, habari na tamaduni za nchi hizo mbili ambapo vyuo hivyo vitaendelea kujifunza kwa pamoja kupitia uzoefu wa hali ya juu na kuimarisha mafunzo na vipaji kwa wanafunzi na wafanyakazi.

Naye Mkuu wa Ofisi ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Chuo Kikuu cha Mawasiliano cha Zhejiang Bw. Guo Liang alieleza kufurahishwa na kuwepo kwa wanafunzi kutoka Zanzibar katika chuo hicho. Aliahidi kutoa ushirikiano zaidi kwa wanafunzi na wafanyakazi wa SUZA na Zanzibar kwa jumla wanaokwenda katika Chuo hicho.

TIKA yafungua milango kuimarisha kilimo SUZA

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kimefanya mazungumzo na Shirika la Ushirikiano na Uratibu la Uturuki (TIKA) kwa lengo la kujenga uhusiano mwema na kuimarisha sekta ya kilimo.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Mipango, Fedha na Utawala, Dkt. Hashim Hamza Chande alisema fursa hii imekuja wakati muafaka ambapo SUZA inaendelea na kutanua wigo wa miundombinu yake sambamba na kuongeza idadi ya wanafunzi.

Aliongeza kuwa SUZA kupitia Skuli yake ya Kilimo iliyoko Kizimbani, kinawapatia utaalumu wa kilimo cha mazao

ya chakula, biashara pamoja na ufugaji kwa wakulima walioko mitaani na wanafunzi.

“Chuo kinawafundisha wakulima wa mpunga kwa makundi pia matumizi ya mbinu bora za kilimo”, alisema.

Naye Mratibu wa Shirika hilo, Bibi Filiz Sahinci, alisema Uturuki kupitia mashirika yake mbali mbali ina uzoefu na utaalumu mkubwa katika masuala ya kilimo.

“Tunataka kujuana shughuli zetu ili tuone fursa ziko wapi ili tuzitumie kwa pamoja, tunajenga marafiki ambao tunafanya nao kazipamoja”, alisisitiza Bibi Filiz.

Aidha, aliongeza kuwa TIKA itatoa fursa ya kuleta wataalamu

wa kilimo na baadaye mafunzo hayo yaendelezwe na wazawa. TIKA ni Shirika ambalo limeanzishwa mwaka 1992 nchini Uturuki na kuanza kazi zake Tanzania mwaka 2017 hadi sasa limekamilisha miradi 300 katika sekta kadhaa zikiwemo ya kilimo, afya, elimu na maji.

Shirika la Ushirikiano na Uratibu wa Kituruki (TIKA) ni idara ya serikali chini ya Wizara ya Utamaduni na Ufalii. Hujishughulisha na ushirikiano wa maendeleo, TIKA inafanya kazi katika nchi zaidi ya 150.

TIKA inawajibika kwa shirika la misaada ya maendeleo la Uturuki kwa nchi zinazoendelea, kwa kuzingatia hasa nchi za jamii ya Kituruki na Afrika.



SUZA yashiriki Maonesho Wiki ya Taifa ya Elimu Tanga

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Prof. Moh'd Makame Haji amesema Chuo kinatumia fursa ya kushiriki maonesho kuongeza wigo wa kupata wanafunzi ili kutoa huduma zake kwa watu wengi zaidi.

Hayo aliyasema katika mahojiano na vyombo vya habari baada ya hafla ya ufunguzi wa Maonesho ya Wiki ya Taifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika katika viwanja vya Skuli ya Sekondari ya Popatlal huko Mkoani Tanga kuanzia tarehe 25 hadi 31 Mei, 2024.

Maonesho hayo yalikuwa na kaulimbiu "Elimu, ujuzinauvumbuzi kwa uchumi wa ushindani". Alifahamisha kuwa dhamira nyengine ni kujumuika na wadau wengine ili kubadilishana uzoefu na kujiongezeza maarifa zaidi sambamba na kudakhili wanafunzi wapya wajiunge na fani mbalimbali zinazotolewa na SUZA

"Tunatoa taaluma na taarifa zinazohusu chuo chetu ili wenye matamano wanaotaka kujiunga wapate fursa hiyo", alifahamisha.

Aliongeza kuwa katika utafiti, SUZA imepata nafasi katika matukio ya kutafiti ili utafiti wake uweze kutumika kama ni sehemu ya kuleta mabadiliko kama ambavyo imeonekana katika matukio mbali mbali ya kijamii huko Zanzibar.

Makamu Mkuu wa Chuo alifahamisha kuwa SUZA inatoa mafunzo kwa programu mbalimbali ambapo utafiti na ushauri ni sehemu ya shughuli zake. "Tafiti hizo miongoni mwao zimetumika na zimewahi kutoa suluhu ya changamoto zinazozikabili jamii".

Aliendelea kuogea kwa kusema kuwa tafiti zinazofanywa na wanafunzi wa SUZA zimejiegemeza kuendana na sera za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kukuza uchumi wa buluu na gesi asilia na kutatua changamoto za jamii.

"Zikipewa nafasi nzuri zitaleta mabadiliko", alisisitiza Alipoulizwa kuhusu kuwa na Kampasi za SUZA Tanzania Bara alijibu kuwa kwanza Chuo kimepanga kutanua wigo wake wa kutengeneza miundombinu hatua inayoendelea ambapo kwa sasa ipo Kampasi moja tu kisiwani Pemba.

Hata hivyo, alisema SUZA imekuwa na utaratibu wa kufanya ziara katika skuli mbalimbali za Tanzania bara kwa ajili ya kujitangaza na kudakhili wanafunzi lakini kuna mpango wa kuanzisha Kampasi Tanzania bara hapo baadaye.

Katika ziara hizo hivi karibuni maofisa wa SUZA walifanya ziara katika skuli za sekondari za mikoa ya Arusha, Mwanza na Tabora. Alisema SUZA imekuwa ikishiriki na kuonesha kazi na huduma zake katika maonesho mara zote ila kwa mara ya kwanza maonesho haya

yamekuwa makubwa zaidi kufuatia taasisi zinazoendesha maonesho hayo za Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) na NACTVET kuungana na kukusanya wadau wengi kwa wakati mmoja.

Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu iliandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST).

Maonesho hayo yameshirikisha taasisi 140 za elimu ya juu. Hafla hiyo ilihusisha juhudi za ushirikiano wa pamoja wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST), Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) pamoja na Maonesho ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Amali, yaliyoratibiwa na Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

Mgeni rasmi katika hafla ya ufunguzi wa maonesho iliyofanyika tarehe 27 Mei, 2024 alikuwa ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda.

Mgeni rasmi katika siku ya kilele na ufungaji alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa tarehe 31 Mei, 2024.

Katika hotuba yake, aliwaeleza washiriki kuwa, serikali inalenga kuanzisha vitengo vya ubunifu na ukuzaji ujuzi kote nchini ili kuwasaidia vijana wenye vipaji na kuchochea ukuaji wa uchumi nchini.



SUZA, washirika kuleta mabadiliko ya kidijitali

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji, ametoa wito kwa washirika wa mradi wa Rehabilitation For All Through Digital Innovation and New Competencies (RADIC) kuwa tayari kujishughulisha na mabadiliko yatakanyo na miradi hiyo kuelekea maendeleo ya nchi za Afrika. Akizungumza kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo, wakati wa uzinduzi wa warsha ya Mitaala kuhusu Digital Rehabilitation Dkt. Hashim Hamza Chande alisema kuwa, mradi huo unalenga kuziwezesha taasisi za elimu ya juu kuwa na uwezo wa kusaidia na kuongeza suluhisho la kidijitali katika eneo zima la Afrika Mashariki, kwenye nyanja za kijamii, afya na elimu. Alieleza kuwa mradi huo uliozikutanisha taasisi za vyuo vikuu kutoka Finland, Tanzania, Kenya, Rwanda na Ujerumani utaleta utaalamu wa kuchunguza fursa za elimu, kukuza ubunifu na kuinua ubora wa elimu. "Utekelezaji wa mradi wa RADIC utaakisi mabadiliko ya kiteknolojia kwa jamii ambayo itawezesha upatikanaji wa elimu kwa urahisi kwa maeneo yaliyo karibu, pembezoni, vijijini pamoja na kugusa maeneo yote ya kijamii," aliongeza. RADIC ni mradi wa miaka mitatu unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya ambao ulianza Machi 2023 na kuendesha kwa pamoja na taasisi nane za elimu ya juu ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikristo cha Tiba cha Kilimanjaro (KCMUCo) (Tanzania), Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Jomo Kenyatta (Kenya),

Chuo Kikuu cha Moi (Kenya), Chuo Kikuu cha Rwanda (Rwanda), Chuo Kikuu cha Global Health Equity (UGHE) Ltd (Rwanda), Chuo Kikuu cha Sayansi cha JAMK (Finland), na Hochschule fur Gesundheit (Ujerumani). RADIC ni mradi wa utafiti wa kuchangia kujenga uwezo katika elimu ya juu ili kusaidia na kukuza mabadiliko ya kidijitali katika Afrika Mashariki. Wakati huo huo, Dkt. Chande alizindua warsha ya mtandaoni na ya Blended Learning and

Science Communication (BLSC) kwa ajili ya kubadilishana uwezo juu ya utumiaji wa mbinu za kisasa ambazo zinasisitiza matumizi ya stadi za karne ya 21. Warsha hiyo iliwakufanisha SUZA, Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikristo cha Tiba cha Kilimanjaro (KCMUCo) - Tanzania, Chuo Kikuu cha Jimma (JU) - Ethiopia na Chuo Kikuu cha Copenhagen (UCPH) - Denmark. Shughulizote mbilizilifanyika katika Taasisi ya Ufalii, Kampasi ya SUZA Maruhubi.

SUZA yahitaji mawasiliano yenye tija

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Maendeleo na ukuaji wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) umelezwa kuwa unalazimisha kuwa na mpango madhubuti wa kisasa wa mawasiliano utakaokiwezesha Chuo hicho kukiunganisha na wadau wa ndani na nje ya nchi.

Akizungumza katika ufunguzi wa kikao cha kupitia sera ya Mawasiliano ya SUZA Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Moh'd Makame Haji, amesema ukubwa wa Chuo na kasi ya maendeleo iliyopo ni vyema kuwa na nyenzo za mawasiliano za kisasa zitakazoleta tija.

"Leo chuo kina kampasi tisa, nane zipo Unguja na moja iko Pemba, kuna wafanyakazi takriban 700 na wanafunzi 7,200 na wanaendelea kuongezeka,

kama hatuna mipago mizuri ya mawasiliano itakuwa shida", alisema Prof. Haji.

Alifahamisha kuwa moja ya maeneo ambayo Chuo kinapaswa kuimarishwa ni kuwa na mawasiliano imara na ya uhakika ambayo yanafuata kanuni za kisasa zinazotambulika.

"Hawatotuona, hawatatujua wala hawatotusikia kama hatujafanya mawasiliano yetu kuendana na wakati uliopo", alisema."

Alieleza kuwa ana matarajio kuwa sera ya mawasiliano ya SUZA inakuwa bora ili kusaidia Chuo na Taifa kujenga misingi bora inayokwenda na wakati.

Warsha hiyo ya siku moja iliwashirikisha wanaSUZA na wanahabari wazoefu wa Zanzibar ilifanyika huko Maruhubi hivi karibuni.



SUZA, EMU waahidi kushirikiana masuala ya kitaaluma

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Eastern Mediterranean University (EMU) cha Cyprus vimekubaliana kuanzisha uhusiano wenye manufaa kwa pande zote mbili kwa masuala ya utafiti na mafunzo, na mipango mingine ya elimu yenye maslahi ya pamoja.

Makubaliano haya yamefikwa tarehe 20 Mei, 2024 kufuatia mazungumzo kati ya Prof. Moh'd

Makame Haji, Makamu Mkuu wa SUZA na Prof. Hasan Kilic, Mkuu wa Chuo wa EMU. Mazungumzo haya yalilenga ushirikiano katika kufundisha wafanyakazi na programu za kubadilishana wanafunzi.

Prof. Makame alimweleza mgeni wake kuwa, miongoni mwa majukumu ya msingi ya SUZA ni kutambua mahitaji ya soko na kuisaidia serikali kupata wafanyakazi wenye sifa. "Uhusiano kama huo kati ya taasisi zetu unaweza

Aliendelea kumfahamisha mgeni wake kuwa kwa sasa watumishi wanne wa SUZA wanasoma nchini Cyprus katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu na wengine watatu wapo nchi Jirani ya Uturuki; wote wanasomea masuala ya utalii na usimamizi wa ukarimu.

SUZA kinatarajia kuwa baada ya wasomi hao kumaliza masomo yao watakuwa na msaada mkubwa kwa SUZA na Taifa kwa ujumla.

"SUZA imefurahishwa na upanuzi wa wigo wa ushirikiano na taasisi yenu, hii itaimarisha na kuwajengea uwezo wafanyakazi na wanafunzi wetu katika kufikia malengo yao, hivyo kuwezesha kupata sifa za kitaaluma kimataifa," alieleza Makamu Mkuu wa Chuo.

Makamu Mkuu wa Chuo aliongeza kusemakuwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sasa imejiimarisha katika ujenzi wa hospitali katika kila Wilaya za Zanzibar ambapo SUZA ina mchango mkubwa katika utoaji wa watumishi wa afya katika fani za ufamasia na maabara za tiba ili kuweza kuhudumia katika hospitali hizo.

Pia alifahamisha kuwa SUZA iko katika mchakato wa usaidizi kwenye matumizi ya digitali kitaaluma na kiuongozi.

Wakati huo huo, Prof. Hasan Kilic, aliarifu kuwa taasisi yake ilianzishwa mwaka 1978 na hadi sasa wahitimu wapatao 35,000 wamehitimu tangu kuanzishwa kwake, alieleza kuwa EMU inasajili wanafunzi wa kigeni kutoka sehemu mbalimbali duniani, aliwataja baadhi yao ni kutoka Rwanda, Kenya na Tanzania ambako ndani yake wapo Wazanzibari.

Alitoa witokwa wanafunzi wa SUZA kujiunga na wanafunzi wengine wa EMU katika kufanya utafiti na kutumia angalau muhula mmoja wa masomo katika taasisi yao.

Prof. Kilic alimhakikishia Prof. Haji kuwa EMU iko tayari kushirikiana na SUZA kwa kuchanganya mitaala yao ya kitaaluma akiamini kuwa kwa kufanya hivyo mafanikio ya pande zote mbili yatapatikana.

Wawili hao walikubaliana kupanua ushirikiano wao katika nyanja za mafunzo ya wafanyakazi, maendeleo ya mtaala, mipango ya kubadilishana wanafunzi, programu za masomo ya shahada za uzamili juu ya mafuta na gesi na programu za pamoja katika fani nyingine za shahada za uzamili na uzamivu.

Mapema, Dkt. Abdulrahim Haroun Ali, Mkuu wa Kituo cha Mafunzo ya Kidijitali (CDL), aliarifu kuwa Kituo kinatarajia kuandaa programu kadhaa zitakazopatikana ndani na nje ya nchi. Aliongeza kuwa programu hizo zitatoa msaada kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na sekondari kwa masomo ya sayansi ikiwa ni pamoja na Biolojia, Kemia na masomo mengineyo.

The Eastern Mediterranean University (EMU) ni Chuo Kikuu cha umma kilichoko Famagusta, Cyprus ya Kaskazini. Kilianzishwa mwaka 1979 kama taasisi ya elimu ya juu ya teknolojia kwa waCyprus wenye asili ya Kituruki na baadaye kubadilishwa kuwa Chuo Kikuu cha serikali ilipofika 1986.

EMU inatoa aina mbalimbali za taaluma kuanzia shahada ya kwanza hadi zile za uzamili na uzamivu. Masomo hutolewa kwa lugha za Kiingereza na Kiruruki.



SUZA, NCT kushirikiana

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) vimetia saini hati ya makubaliano ya mashirikiano kati yao yakiwa na lengo la kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kitaaluma katika fani za utalii na ukarimu

Hati hiyo ya makubaliano imekuja baada ya kuona juhudi kubwa zilizofanywa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan na Mhe. Dk Hussein Mwinyi katika kuhamasisha na kutangaza sekta ya utalii kupitia Filamu za Tanzania za Royal Tour na Amazing Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa Habari jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dkt. Florian Mtei amesema NCT na SUZA zimekubaliana kushirikiana katika masuala ya taaluma kwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa wadau waliopo kwenye mnyororo wa thamani wa utalii.

“Tanzania ina vivutio vingi vya utalii ambapo juhudi kubwa zimeendelea kufanywa na marais wetu wawili katika kutangaza utalii na fursa za uwekezaji hapa Tanzania. Hivyo sisi wanataaluma tukaona tuendelee kuungamkono juhudi zao na kuhakikisha kwamba tunatoa elimu ya utalii na ukarimu kwa viwango vya kimataifa”, alisema Dkt. Mtei.

Aidha Dkt. Mtei alisema kwamba vyyo hivyo vimekubaliana kuwa na programu maalum ya kubadilishana wanataaluma na wanafunzi kati yao. Aliendelea kusema kuwa, vyyo hivyo vitafanya ushirikiano kwenye maeneo mengine yakiwemo kutafuta maeneo ya kufanya mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya wanafunzi wa taasisi hizo na kuandaa mashindano mbalimbali kwenye fani ya upishi ambapo tayari NCT na Taasisi ya Utalii Zanzibar zimekwishakufanya hivyo.

Aidha Dkt. Mtei alisema wao kama NCT kwa kushirikiana na SUZA zitashirikiana kuandaa Tamasha la Chakula ambalo litalenga kutangaza aina zote za vyakula vya asili vya Tanzania Bara na Zanzibar.

“Hiyo yote ni kutangaza vivutio vyetu vya utalii kupitia Utalii wa Kiutamaduni kupitia Tamasha hilo”, aliongeza Dkt. Mtei.

Mbali na hayo, Dkt. Mtei alisema kupitia ushirikiano huo wataandaa kongamano kubwa la kimataifa litakalofanyika tarehe 21 na 22 Novemba mwaka huu jijini Arusha, hivyo aliikaribisha SUZA kushiriki na kutoa mada mbalimbali kuhusu uchumi wa Buluu.

Kwa upande wake Prof. Moh'd Makame Haji, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar alisema kuwa, Tanzania bara

na Zanzibar zimeona jitihada nyinigi zimefanyika katika kuimarisha sekta ya utalii, hivyo zitahakikisha sekta hii inaingia kwenye mpango mkakati wa serikali na kuiwekea sera maalum ili kuimarisha uchumi.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amekuja na Sera ya Uchumi wa Buluu, ambapo utalii ni miongoni mwa sekta muhimu zinazosimamia sera hiyo. Utalii una mchango mkubwa wa kuliingizia taifa letu pato na fedha za kigeni pamoja na kusaidia jamii ya Kitanzania kuweza kupata fursa mbalimbali zinazotokana na shughuli za utalii kama vile ajira na shughuli nyengine zinawapatia kipato. Sekta hii nayo imewekwa katika mpango maalum”, alisema Prof. Makame.

Aliongeza kuwa, Uchumi wa Buluu kwa upande wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ni eneo ambalo linaimarika kwa kasi, na hiyo inatokana na juhudi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Taasisi zetu za Taaluma zinajikuita ziko nyuma kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na juhudi za serikali zetu katika kuendeleza mbele maendeleo ya sekta ya utalii.

Hili limetufanya tukae kwa pamoja ili kujitathmini na kuangalia mikakati iliyo bora ya kuongeza nguvu na kufanya kazi kwa pamoja ili kuimarisha sekta ya utalii.



Ondosheni vikwazo vya utoaji elimu - Lela aagiza

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Lela Muhammed Mussa ameziagiza taasisi zote zinazohusiana na utoaji elimu kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa iwe ni jumuishii na kusiwe na wa kuachwa nyuma katika mapokezi ya elimu inayotolewa.

Mhe. Lela aliyasema hayo wakati akifungua semina kuhusu Kuvunja Vikwazo vya Elimu kwenye Usumeshaji Ujumuishaji na Matumizi ya Teknolojia iliyofanyika katika Kampasi ya Maruhubi tarehe 9 Septemba, 2024.

Alielezakuwa warsha hii inaendana na mageuzi ya kielimu yanayofanyika sasa katika mfumo wa elimu Tanzania.

“Warsha tunayozindua leo ni sehemu ya mpango mpana wa Kuvunja Vikwazo vya Elimu kwenye Usumeshaji: Ujumuishaji na Matumizi ya Teknolojia”, alisema.

Aliendelea kufahamisha kuwa mradi huu umejikita katika kuimarisha uwezo wa taasisi za elimu ya juu kote Afrika Mashariki ili kuwa karibu na kuhakikisha ushirikishwaji wa watu wenye mahitaji maalum sio tu katika elimu bali katika masuala yote ya kijamii nzima.

“Kiini cha mpango huu ni imani kwamba elimu ni haki ya msingi ya binadamu, warsha hii inatoa fursa ya kujifunza kutoka kwa kila mmoja na kujenga mtandao wa wataalamu waliojitolea kukuza elimu jumuishii”, aliwaambia washiriki wa warsha.

Katika kusisitiza umuhimu wa elimu, Mheshimiwa Lela alisema kwa muda mrefu tumelewa nguvu ya elimu katika kuunda mustakabali na kuwezesha vizazi, hii ni hatua nyingine muhimu mbele kwa kutambua kuwa elimu jumuishii sio anasa bali ni hitaji la lazima.

Ilielezwa kuwa moja ya shughuli muhimu zinazopaswa kuzingatiwa katika mradi huu ni mapitio ya mitaala ya elimu na ufundishaji ili kuwa jumuishii kwa wenye mahitaji maalum.

“Hii sio kazi ndogo, na tunajua kabisa changamoto zinazojitokeza.

Itahitaji mabadiliko katika njia tunazotumia kufundisha na kujifunza. Itahitaji mabadiliko katika mawazo, miundombinu na mbinu. Lakini muhimu zaidi, itahitaji juhudi za pamoja ili kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi bila kujali uwezo, ana nafasi ya kustawi”, alisema Mhe. Lela.

Iliarifiwa kuwa ufundishaji jumuishii utaunda mazingira ya kujifunza ambapo wanafunzi wote, ikiwa ni pamoja na wale wenye mahitaji maalum, watathaminiwa na kuungwa mkono; kubuni mitaala inayoakisi utofauti na kuhakikisha mbinu za kufundisha zinakidhi mahitaji na uwezo tofauti.

Njia hii haitawanufaisha wanafunzi wenye mahitaji maalum tu bali pia kuongezauzoefuwakujifunzawakilamtu. Mhe. Lela aliendelea kuwaambia washiriki wa warsha hiyo kuwa amefurahi sana kuona lengo la teknolojia saidizi na mbinu za ubunifu za ufundishaji, ambazo zina uwezo wa kubadilisha uzoefu wa kujifunza wa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Kwa kukumbatia teknolojia na mbinu hizi, tunaweza kuunda mazingira ya kujifunza zaidi na wezeshi ambayo yanakidhi mahitaji mbalimbali ya wanafunzi wote.

“Kupitia zana za ubunifu na matumizi ya kidijitali, tunaweza kuziba mapengo katika upatikanaji wa elimu, kuongeza njia za kujifunza, na kuwawezesha walimu kuunda mazingira ya kujifunza yanayoweza kubadilika na ya uwazi, lakini teknolojia pekee haitoshi kwani lazima iunganishwe na juhudi na umakini, vitendo jumuishii, na kujitolea kukuza mazingira ya kuheshimiana na kuwathamini wanafunzi wote” alijulisha Mhe. Lela.

Warsha hii ambayo ilikusanya wataalam, waelimishaji na viongozi wenye kujali ushirikishwaji wa wenye mahitaji maalum katika elimu walichangia maarifa, kubadilishana mawazo na mikakati ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa taasisi zetu ziko tayari kukidhi mahitaji ya wanafunzi wote.

Alisema kuwa uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kujitolea kwa waelimishaji na taasisi katika kanda nzima vinaweza kujenga mazingira ya elimu jumuishii na usawa. Alitoa shukrani

zake kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa msaada wake usioyumba na kujitolea katika maendeleo ya elimu kwa wale wenye mahitaji maalum.

Alihitimisha kwa kusema kuwa ana imani kwamba kwa pamoja wote wanaweza kupiga hatua kubwa katika kuvunja vikwazo vinavyozuia watu wenye mahitaji maalum kupata elimu wanayostahili.

Makamo Mkuu wa Chuo cha SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji ameeleza kuridhishwa kwake na ushirikiano uliopo baina ya wa washirika wa maendeleo na SUZA kwenye miradi ya ubunifu ambayo imekuwa ni ushahidi wa utekelezaji wa majukumu yake kimataifa na kubadilishana uzoefu,

Alisema, tangu Chuo kilipoanza kutoa huduma mwaka 2001 kimekuwa kikiendelea kutoa elimu ya juu kupitia kozi zake na program mbali mbali wa watu wa Zanzibar na nje na kimekuwa kikichangia sana ukuaji wa uchumi.

Lengo la mradi wa BERT ni kuongeza uwezo wa vyuo vikuu vya Afrika Mashariki kuondoa vikwazo mbalimbali (ikiwemo digitali) ambavyo vinazuia ushirikishwaji na ushiriki wa watu wenye ulemavu katika jamii.

Mradi huo unasaidia vyuo vikuu vya washirika katika kukuza huduma za ukarabati wa aina mbalimbali, upatikanaji wa masomo, na matumizi ya vifaa vya teknolojia katika kufundisha wanafunzi wenye ulemavu.

Zaidi ya hayo, mradi huo una lengo la kuinua kiwango cha elimu na utaalumu wa vyuo vikuu vya washirika katika kuendeleza mazingira ya kujifunza na kufundisha bila kizuizi.

Mradi huu umefadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Finland, na kusimamiwa na Shirika la Taifa la Elimu la Kifini (EDUFI), mpango wa Ushirikiano wa Elimu ya Juu (HEP) inasaidia ushirikiano kati ya vyuo vikuu vya Finland na nchi zinazoendelea.

Mradi wa BERT ni sehemu ya mpango wa HEP, ambao pia unaendana na malengo ya mpango wa serikali ya Finland ili kuimarisha ushirikiano wa Finland.



Ziara za kimasomo SUZA, Østfold Norway zaimarika

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kimewateua wanafunzi wanne wanaosomea Stashahada ya Elimu ya Awali na walimu wawili kufanya ziara za kimasomo nchini Norway. Aidha, wanafunzi wengine watano na walimu wawili wataoka Norway kuja Zanzibar kwa lengo la kubadilishana utaalamu.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya SUZA kupitia Skuli ya Elimu na Østfold University College kutiliana saine ushirikiano tangu mwaka 2019, makubaliano yanayojulikana kama NoZa Intercultural Mobility.

Wakiwa Norway wanafunzi hao watapata fursa ya kutembelea sehemu mbalimbali pamoja na kuhudhuria masomo darasani.

Akizungumza katika hafla ya kuwaaga wanafunzi hao, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinaimarisha elimu kwa kuweka mazingira ya kuwawezesha vijana kujiunga na vyuo vya elimu ya juu nchini.

“Programu zinapata nguvu kubwa na ushawishi, tuna uhitaji mkubwa na kwa vile elimu haimuachi mtu nyuma, ndio maana tunashajiisha kupatikana fursa hizi”, alisema.

Kutokana na umuhimu wa masomo hayo na mahitaji ya nchi kwenye taalumahiyu, Prof. Hajialiwashauri wanafunzi kuzitumia vyema fursa hizo ili kufikia malengo yaliyowekwa.

“Masomo hayo ni adimu lakini ni muhimu katika sekta ya elimu kwani hatuna wataalamu wa kutosha ambapo awali hatukuweka mazingira ya kupatikana wataalamu kwenye fani hiyo”, alisema Prof. SUZA kina mipango mingi miongoni mwao ni kufanya makubaliano ya ushirikiano baina ya Zanzibar na Norway ambako wakienda watakutana na wanafunzi kutoka mataifa mengine na wanapaswa wajifunze mazingira na utamaduni wenye maadili mema.

Aidha, aliwaonya wanafunzi hao kwa kuwaambia kuwa SUZA haiko tayari kuharibu uhusiano uliopo kwa wanafunzi kwenenda na kuamua kutorudi nyumbani kwa kuamua kulowea huko hivyo kukivunja heshima Chuo, SUZA haiko tayari hayo kutokea.

Mapema, Mkuu wa Skuli ya Elimu Dkt. Said Khamis Juma, alifafanua

kuwa mnamo mwaka 2022 wanafunzi wanne kutoka Diploma ya Elimu Mjumuisho na Mahitaji Maalum na Diploma ya Elimu ya Awali, walishiriki katika ziara hiyo na mwaka 2023 wanafunzi sita wa Shahada ya Uzamili ya Elimu kwenye sekta ya Vijana, Jinsia na Maendeleo walitembelea Chuo cha Østfold kwa muda wa wiki tatu.

Wazazi wa wanafunzi ambao walishiriki katika hafla fupi ya kuwaaga wanafunzi hao iliyofanyika kwenye ofisi za SUZA, huko Tun-guu waliushukuru uongozi wa Chuo kwa kuwasimamia vyema wanafunzi. Kwa niaba ya wenzake Mzee Mussa Salum aliwanasihi wanafunzi hao kufuata maelekezo waliyopewa.

Chuo Kikuu cha Østfold kinapatikana Wilaya ya Østfold, Norway. Ni miongoni mwa vyuo vikuu vya umma nchini Norway, na ni matokeo ya vyuo vitano vya umma huko Halden, Sarpsborg na Fredrikstad ambavyo viliunganishwa pamoja kama sehemu ya Mageuzi ya Chuo Kikuu yaliyofanyika 1994.

Chuo hiki hutoa zaidi ya nyanja 60 za utafiti, kuanzia Shahada Mshiriki (Associate degrees), Shahada (Bachelor's degrees), Shahada za Uzamili na baadhi ya Shahada za Uzamivu.



Uwajibikaji kwa wakati huondoa changamoto - PAC

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Kamati ya Hesabu za Umma (PAC) ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imekisha Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kuufanyia kazi kwa wakati ushauri unaotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuepusha changamoto zinazoweza kutokea.

Hayo yamesemwa na Kamati hiyo wakati wakijadili kwa pamoja na SUZA kuhusu ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Fedha na Hesabu za Serikali mwaka 2021/2022 za mfumo wa TEHAMA kwenye kikao kilichofanyika makao makuu ya SUZA huko Tunuu, Wilaya ya Kusini Unguja.

Kamati hiyo imekiri kuwa, SUZA imeshauriwa mambo mengi ambayo yanalenga kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake kwa maendeleo ya SUZA na endapo yatafanywa kazi kwa haraka mafanikio yatapatikana.

“Mambo yakichukuliwa hatua kwa haraka yatapunguza athari zinazoweza kutokea. CAG anapopita na kushauri kila wakichelewa watazifanyia kazi kama zimamoto na hakutakuwa na mafanikio,” alisema Mhe. Mohammed Abdallah Salum, mjumbe wa PAC.

Mapema, Makamu Mkuu wa

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji, alikiri kuchelewa kuungwa mkonga wa Chuo kulitokana na baadhi ya Kampasi za Chuo kutokuwepo wakati wa kuunganishwa mfumo huo.

“Uendeshaji wa mfumo una changamoto nyingi na taasisi za elimu zinahitaji mfumo bora jambo ambalo limefanyiwa kazi, mkonga umeungwa na huduma za mfumo zinapatikana kama kawaida”, alisema Prof. Haji.

Akijibu suali kuhusiana na bajeti na uendeshaji wa Chuo, Prof. Haji. alithibitisha kuwa unaenda vizuri kwani chuo kimeweza kulipa madeni yote kutoka mwaka 2014 hadi 2024 na madeni yaliyobaki ni yale ambayo yako kwenye mkataba kama vile ujenzi wa nyumba katika kampasi za Mbwenina Dakhalia huko Chwaka. Naye, Mhandisi Robert Mwelo,

Mkaguzi wa mifumo ya Serikali, alisema SUZA ina jamii kubwa ya wanafunzi na wafanyakazi wakiwemo wahasibu ambao wanahitaji huduma hii muhimu katika kutekeleza majukumu yao.

Aidha, alihimiza kupewa kipaumbele bajeti ya mifumo ya TEHAMA ili kukabiliana na changamoto za kupatikana huduma za mtandao.

“Ikikosekana huduma hii wanafunzi hawawezi kujifunza na wahasibu nao watahindwa kufanya kazi zao kwa wakati”, alikumbusha.

Kwa upande wake, mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Juma Ali Khatib alisema, Kamati imeridhishwa na utendaji wa SUZA kwa kujibu kwa ufasaha hoja zote zilizowasilishwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

“Chuo kinategemewa na watu wengi ndani na nje ya nchi na tunakitarajia kuwa ni kivutio kwa watu wote katika utoaji wa elimu bora”, alifahamisha.

Kuhusu ufuatiliaji wa mfumo, alishauri kufuatilia ubora wake kwa kupitia hatua stahiki na kwa kufuata taratibu zote pamoja na kufanyiwa majaribio na kupokea maoni ya watuamiaji ili kuhakikisha kuwa mfumo huo upo vizuri kimatuzi.

Kamati ya Hesabu za Umma (PAC) ni Kamati ndani ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambayo jukumu lake ni kusoma ukaguzi wa matumizi ya fedha za umma, kuwaalika mawaziri, makatiibu wakuu au maafisa wengine wa wizara kwenye kamati kwa ajili ya kuhojiwa, na kutoa ripoti juu ya matokeo yao baada ya ukaguzi wa bajeti ya serikali. PAC inachunguza akaunti za serikali kwa misingi ya ripoti za CAG.



Mikakati kuanzisha Masomo Sayansi ya Bahari yawekwa

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji amekutana na wataalamu wa masuala ya bahari kwa ajili ya kujadili namna bora watakaavyoweza kuendesha taasisi ya masomo ya bahari katika hatua za awali.

Mazungumzo hayo yalifanyika katika ofisi ya Makamu Mkuu wa Chuo, Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja tarehe 29 Mei, 2024. Katika mazungumzo hayo, Prof. Haji aliwaeleza wataalamu kuwa, SUZA imepiga hatua za kuanzishwa kwa Taasisi itakayotoa mafunzo ya bahari ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko nyuma ya mpango huo.

Aidha, alifanua kuwa SUZA inaendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na wadau wanaoshughulikia masuala ya bahari na Uchumi wa Buluu kwa jumla. “Katika nyanja hii tunataka kutengeneza vipaji vinavyohitajika ikiwa ni pamoja na wahandisi, wataalamu katika uzamiaji, wataalamu masuala ya hali ya hewa, na fani nyengine zinazohusiana na masuala ya uchumi wa buluu katika viwango vinaavyokubalika kimataifa”, alisitiza.

“Tunataka kuwafundisha watu programu za kuwajengea uwezo ili watumie ujuzi kwa ajili ya kufanya kazi kufikia malengo ya uzalishaji wa uchumi unaotarajiwa na Serikali yetu.”, alisema.

Aidha, alifahamisha kuwa, mafanikio makubwa yanatarajiwa kufikiwa iwapo SUZA itakashirikiana na wadau wengine katika suala hili. Akiwasilisha muongozo wa mpango wa kuanzishwa Tume ya mafunzo ya Bahari, Mkuu wa Idara ya Sayansi ya Bahari ya SUZA, Dkt. Yahya Sheikh alisema kuwa wanafunzi wanane wanatarajiwa kupata mafunzo juu ya masuala ya bahari nje ya nchi.

“Tukitaka watendaji wazuri zaidi ni lazima wajifunze kwa watu wengine wenye utaalamu unaofanana na taaluma wanayotarajia kuifanyia kazi, tunawatarajia sana katika ukuzaji wa mitaala ya taasisi hii”, alisema.

Aliendelea kuongeza kwamba taasisi ina matarajio ya kuanza mafunzo ya Bahari na wanafunzi elfu moja, pia wana matarajio ya kuanzisha kitu kingine cha mafunzo hayo huko Pemba. Alisema kupitia programu hizo wanatarajia kukuza biashara ya mwani huko Pemba ambako kilimo hicho kinastawi zaidi.

“Haya ni miongoni mwa mambo yatakayoinufaisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tukizungumzia masuala ya Uchumi wa Buluu bila kuwa na mafunzo aina hii hilo ni tatizo”, alisema Dkt. Yahya Sheikh.

Kwa upande wao, Kiongozi wa msafara huo, Kamanda Pepijin Verstand na mwenzake Ericjan de Roode kutoka Maritime Capacity Alliance, Uholanzi wamefurahishwa na hatua za SUZA za kuanzisha Taasisi itakayotoa

mafunzo ya masuala ya bahari. Mapema, Kamanda Pepiji alitoa mwelekeo wa kuanzisha Taasisi ya mafunzo ya awali kwa makamanda nchini ifikapo Juni mwaka huu kwa kutoa vigezo vya msingi na kuisisitiza kuwa uanzishwaji wa Taasisi inafaa ufanywe hatua kwa hatua.

“Tunategemea Tanzania itakuwa nchi kubwa katika masuala ya bahari ila kwa kuzingatia masuala ya sheria na viwango vya kimataifa, tunaweza kuwaleta walimu kuwafundisha wazawa,” alisema Kamanda Pepijin.

Aidha, aliongeza kuwa suala la usalama katika bahari ni la msingi kwani linaweza pia kuwa chachu kwa usalama wa watalii, kupambana na magendo na kutambua meli zote zinazopita katika eneo linalohusika. Ni vyema bahari ikatumiwa kwa faida kwani nchi zote zenye bahari duniani zinazalisha fedha kutokana na uchumi wa buluu.

Katika mkutano huu baina ya watendaji wa SUZA na Maritime Capacity Alliance kuli kuwa na majadiliano juu ya namna ya utoaji mafunzo ya bahari miongoni mwao ambayo yatahusisha usalama wa bandari na vyombo vya baharini, nidhamu za mabaharia, kuandaa mtaala wa masomo kushirikiana na taasisi nyengine zinazojishughulisha na masuala ya bahari, kuwaandaa walimu wazawa, viwango vya wanafunzi kuanza mafunzo yao bila kuwasahau wananchi na wavuvi na umuhimu wa kuwa na mkakati wa mawasiliano.



SUZA, HNU waimarisha uhusiano

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Ujumbe kutoka Chuo Kikuu cha Hunan cha China (HNU) ukiongozwa na Makamu wake wa Rais Dkt. Wang Weibin, umefanya ziara ya kikazi katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ili kuongeza fursa za ushirikiano kati ya vyuo hivi. Uhusiano huu unatarajiwa kutoa kipaumbele kwa maeneo mbalimbali yanayohusiana na ufundishaji, utafiti na ushauri, ambapo pia kutakuwa na maeneo mengine mengi ambayo vyuo hivi vimepanga kutanua ushirikiano. Akichangia katika mazungumzo hayo, Makamu Mkuu wa SUZA Prof. Moh'd Makame Haji alisema kuwa amefurahishwa na uhusiano huu ulioanzishwa ambao unatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa na maendeleo. "Ninaamini ushirikiano wetu unaweza kuleta faida kwa pande zote za ushirikiano, kuimarisha nyanja ya ukuzaji elimu kwa wanafunzi wetu pamoja na kuchangia maendeleo ya jamii," aliongeza. Prof. Haji amesema pamoja na kuongezeka kwa idadi ya vijana wanaohitaji ajira, SUZA imekuwa ikiwajengea uwezo kwa kuwapatia ujuzi katika maeneo mbalimbali yakiwemo ujasiriamali ambapo anaamini kuwa ushirikiano huo utaleta manufaa katika taasisi hizo kwa kuongeza ujuzi na utaalamu pamoja na uimarishaji maendeleo ya jamii. Kwa upande wake, Makamu wa Rais wa Chuo Kikuu cha Hunan, Dk. Wang Weibin alisisitiza kuwa mawasiliano ni jambo muhimu kwa HNU na SUZA kwa kuwa jambo hilo linaweza kuchangia kuongeza maarifa, kubadilishana uzoefu na kujifunza tamaduni za pande husika. Dkt. Wang Weibin alieleza kuwa wanafunzi wa Kitanzania, walianza kudahiliwa katika HNU

tangu mwaka 2014 na ushirikiano unaendelea kwa lengo la kuendeleza mpango wa pamoja wa utafiti kati ya walimu wa China na Tanzania. "HNU inawafundisha wanafunzi wengi katika nyanja mbalimbali. Ni matumaini yangu ushirikiano wetu utakuwa na tija zaidi kwa kuleta muendeleo wa yale tunayoyafanya Tanzaniahususan Zanzibar," alisema. Akizungumzia kuhusu Taasisi ya Uchumi, Biashara na Utafiti ya Afrika, Dkt. Wang Weibin alisema kuwa taasisi hii ilianzishwa kwa lengo la kuleta mawasiliano ya karibu na uhusiano mzuri na vyuo vingine vya Afrika.

Chuo Kikuu cha Hunan (HNU) kinapatikana Changsha, mji mkuu wa Mkoa wa Hunan, nchini China, mji ambao ni maarufu kwa historia na utamaduni ambapo uko karibu na Mto Xiangjiang pia Mlima wa Yuelu.

Chuo Kikuu cha Hunan (HNU) ambacho kilianzishwa mwaka 976 AD, ni taasisi ya elimu ya juu iliyoendeshwa kwa muda mrefu zaidi nchini China ambapo imekuwa ikiendeleza elimu ya kitamaduni kwa miaka mingi na imekuwa mfano katika maendeleo ya elimu ya juu ya China.

Kiswahili kimekuwa bidhaa bora duniani

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji, amesema kuwa lugha ya Kiswahili imekuwa bidhaa bora duniani kutokana na umuhimu wake. Amesema kutokana na umuhimu huo, kimekuwa kikifundishwa kwenye vyuo vikuu mbalimbali duniani, kutumika kwenye biashara na matangazo ya vyombo vya Habari vya kitaifa na kimataifa.

Prof. Haji aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na mabalozi wa Ufaransa na Ujerumani waliofika nchini kwa ziara ya wiki mbili kwa ajili ya kujifunza historia ya Zanzibar na ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi Tanzania.

Aidha aliuambia ujumbe huo namna nchi mbalimbali zinavyofanya juhudi za kukiimarisha Kiswahili katika nchi zao ambapo alisema hivi karibuni vyuo kutoka Nigeria na Afrika Kusini vilitembelea Zanzibar kutafuta ushauri wa namna ya kuimarisha lugha hiyo katika nchi zao ikiwemo kuandaa mitaala.

"China ina vyuo vikuu na vyombo vya habari vinavyotumia lugha hiyo lakini pia wafanyabiashara wa Zanzibar wanazungumza lugha hiyo", alisema Makamu Mkuu wa Chuo. Prof. Haji aliongeza kuwa kuna fursa

nyingi za kiuchumi na kibishara kwa hivyo SUZA inataka kusaidia kukuza fursa hizo kwa kukiimarisha Kiswahili hasa kwa kutumia TEHAMA, ili kuwafikia watu wengi zaidi duniani. Akizungumzia historia ya lugha hiyo Tanzania, alisema kama kuna jambo ambalo Hayati Mwalimu Nyerere, Baba wa Taifa alifanikiwa, ni kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa kati ya lugha za makabila zaidi ya 125 yanayopatikana Tanzania.

Prof. Haji alifhamisha kuwa mbali na kuwa Kiswahili ni lugha ya kazi katika nchi za Umoja wa Afrika pia karibu nchi zote za Afrika zinazungumza kughahiyo.

"Kiswahili ni tafauti na lugha nyengine kama vile Yoruba ambazo pamoja na kuwa na wazungumzaji wengi lakini zinazungumzwa katika eneo moja tu ndani ya Nigeria", alisema Makamu Mkuu wa Chuo.

Mapema, Kaimu Mkuu wa Idara ya Kiswahili kwa Wageni Bi. Ziada Tajo Ameir, alisema ujumbe huo wa watu nane umejifunza lugha ya Kiswahili katika maeneo ya siasa na dini ya Kiislamu, utawala wa kisiasa wa Zanzibar kabla na baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 hadi kufikia uongozi wa vyama vingi.

Maeneo mengine waliyojifunza ni haki za binadamu na nafasi za wanawake katika uongozi kwenye Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Lela asifu Vyuho kuanzisha madarasa ya Confucius

Na Mwandishi Wetu, SUZA

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Lela Muhammed Mussa amekipongeza Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Chuo Kikuu cha Zhejiang Normal (ZJNU) kwa msaada mkubwa waliutoa katika ujenzi wa Darasa la Confucius. Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa darasa la mafunzo ya lugha ya Kichina (Confucius) hapa Zanzibar uliofanyika katika Kampasi ya Maruhubi ya SUZA, Mhe. Lela alisema kuwa kuanzishwa kwa programu ya kujifunza lugha ya Kichina ni ishara ya uhusiano wa karibu kati ya China na Zanzibar na ni ishara ya urafiki na ushirikiano ambao umekuwapo kwa muda mrefu. Mhe. Lela alisema kuwa darasa la Confucius lililopo SUZA litatoa ujuzi wa lugha ya Kichina kwa wanafunzi wa Stashahada na Shahada waliopo SUZA na taasisi nyingine mbili za elimu ambazo ni Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) na Skuli ya Leera ambazo zimejiunga na programu hiyo mwaka huu. “Nina matumaini makubwa kuwa mpango huu utaimarisha uhusiano wa kihistoria kati ya Zanzibar na China,” alisema. Aliongeza kuwa lugha ya Kichina imekuwa maarufu duniani kote na kuingizwa katika mfumo wa kitaifa wa elimu katika nchi 85 wakati zaidi ya vituo vya upimaji wa ustadi wa lugha ya Kichina 1,300 vimeanzishwa katika nchi 160. Hata hivyo, aliutaka uongozi wa SUZA kuhamasisha skuli zaidi kujiunga na mafunzo ya lugha ya Kichina ili kuimarisha uhusiano kati ya China na Zanzibar. Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Moh’d Makame Haji aliwataka viongozi wenzake wa serikali, jumuiya ya wafanyabiashara na vijana kujifunza lugha na utamaduni wa Kichina ili kuwawezesha kukabiliana kikamilifu na

chagamoto za karne ya 21. “Niwaombe wajasiriamali wote wa Zanzibar waje kujiunga na mafunzo ili wawe sehemu ya wanufaika waanzilishi wa kile SUZA inachotoa,” alisisitiza.

Akizungumzia uhusiano huo, Makamu Mkuu wa Chuo alisema kuwa uhusiano wa kindugu kati ya China na Tanzania umeimarika zaidi kuliko wakati mwingine wowote.

“Chini ya mwongozo wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika

na mipango yake ya utekelezaji, ushirikiano wa kirafiki kati ya China na Tanzania umepiga hatua kubwa na kuandika ukurasa mpya unaohusisha usawa wa kisiasa na kuaminiana kiuchumi na kitamaduni,” alisema.

Akizungumza katika mkutano huo, Mwenyekiti wa Baraza la ZJNU Prof. Jiang Yunliang aliushukuru uongozi wa SUZA kwa msaada wao kuelekea uanzishwaji wa darasa la mafunzo ya lugha na utamaduni wa Kichina Chuoni hapa.

Sura mpya SUZA, Tunguu yaja

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Profesa Moh’d Makame Haji, amesema Chuo kipo katika mchakato wa mabadiliko ya miundombinu kwa kuandaa mpango mkuu wa mageuzi wa utanuzi wa SUZA wa miaka 20 ijayo. Alisema mpango huo utaongeza nguvu ya kufanya kazi na kwenda sambamba na mabadiliko na kufkia matumaini ya viongozi wakuu wa nchi ya kutaka kuona taasisi zinafanya kazi kwa ufanisi na zinaleta manufaa wakati huu hapo baadaye.

Akizungumza katika kikao cha kupitia sera ya mawasiliano, Makamu Mkuu wa Chuo alisema Chuo kitajenga majengo ya kisasa ambayo yatatoa fursa ya kutumiwa na wataalamu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu.

Aliitaja miradi ambayo inatarajiwa kuleta mageuzi makubwa ni Mradi wa wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET) ambao utajenga majengo ya kisasa ikiwa ni pamoja na maabara kubwa ya kisasa na dakhalia za wanafunzi wa kike na wa kiume pamoja na majengo ya Skuli ya Kilimo.

Alifahamisha kuwa mradi mwingine unaofadhiliwa na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

inawekeza asilimia 10 ya mradi huo ili kujenga majengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na viwanja vya michezo.

“Kwa vile SUZA inashiriki katika sekta ya michezo hivyo, Chuo kitajenga viwanja vya michezo vyenye viwango cha Olimpiki pamoja na nyumba za makaazi za wafanyakazi,” alisema. Aidha, kutakuwepo na kumbi za kisasa na kutoa huduma mbalimbali kama vile maegesho, sehemu za kupata huduma za chakula na maduka makubwa ambayo pia yatakodishwa.

“Hadi tukimaliza tutakuwa tumejenga majengo 39 ambapo skuli zote zilizo chini ya Chuo na nyengine ambazo hazijaanzishwa lakini zimetajwa pia zitajengwa.” Alifahamisha. Aliwahimiza wadau kutoa ushirikiano mkubwa kwa kila mmoja kuwa sehemu ya chuo ili kutoa mwelekeo wa kule chuo kinakotaka kwenda. Tunataka kutengenza Chuo chenye ubora ili kuendana na dira na dhamira yake, aliongeza.

Mwaka jana SUZA iliingia katika vyuo vikuu bora barani Afrika vilivyochaguliwa kutokana na ubora wa kazi vinavyofanya kwa kushika nafasi ya 157 kati ya vyuo 200 licha ya uchanga wake kulinganisha na vyuo vingine. “Hii si nafasi ndogo ikilinganishwa na vyuo vikuu vilivyoko Barani Afrika 1,274,” alisema Makamu Mkuu wa Chuo.



SUZA waandaa sherehe za mahafali kwa Wanafunzi wa Oregon

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Idara ya Kiswahili kwa Wageni ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) tarehe 8 Agosti, 2024 ilifanya Mahafali ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Oregon cha Marekani baada ya kuhitimu masomo yao ya lugha ya Kiswahili Chuoni hapa. Mahafali hayo yalifanyika katika Kampasi ya Vuga. Sherehe hiyo ya Mahafali ilijumuisha wanafunzi 8 ambao walifanikiwa kukamilisha programu ya wiki saba katika viwango vya msingi na vya juu.

Nae Mkuu wa Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Dkt. Abubakar Makame Fakihi, ambaye alikuwa ndiye mgeni rasmi katika Mahafali hayo kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo alipongeza juhudi za wahitimu hao kwa kukamilisha masomo yao ya Kiswahili na utamaduni wake kwa mafanikio.

Pia alisema muda mfupi waliotumia kuwepo hapa SUZA umeweza kujenga mazoweza ambayo si rahisi tena kutoweka. Aliendelea kusema kuwa hatua waliyopiga inahitaji kuendelezwa, hivyo aliwasilhi katika hatua nyingine ya muendeleo wa masomo ya lugha ya Kiswahili kurudi tena SUZA kuendeleza taaluma hii ya lugha ambayo sasa ni lugha inayotambulika kimataifa.

Mkuu wa Skuli pia hakuacha kuzishukuru familia za wanafunzi kwa kuishi vyema na wanafunzi hao huko majumbani kwa kuzingatia mila halisi za Kiswahili. Alitoa wito kwa wanafunzi hao kuwa ni mabalozi wazuri wa kuitangaza SUZA, Zanzibar na Tanzania kwa ujumla pamoja na kuelezea ukarimu na amani iliyopo Zanzibar.

Alimazia kwa kuwatakiwa safari njema wanafunzi hao na kufika salama huko waendako. “Nakutakieni mafanikio makubwa na furaha katika miaka ijayo,” aliwaambia.

Mapema, Mkuu wa Idara ya Kiswahili kwa Wageni Bi. Shani Suleiman Khalfan alitoa shukurani kwa wote walioshiriki katika Mahafali hayo.

Bi. Shani aliwaambia wahitimu kuwa hakuna kitu kigumu zaidi katika maisha kuliko kusema kwaheri kwa mtu au watu ambao umezoweana nao. Tungependa kuwa pamoja nanyi kila wakati, lakini hali hairuhusu.

“Leo sio mwisho wa uhusiano wenu na sisi hapa katika Idara ya Kiswahili kwa Wageni. Baada ya mahafali haya, mtaungana nasi kama ni washirika mliopitia Idara ya Kiswahili kwa Wageni, hivyo kuungana na mamia ya wengine waliopitia hapa kutoka pande zote za dunia”, alisema.

“Tunatarajia kwamba mtaendelea kujifunza lugha na utamaduni wa Kiswahili katika vipindi vya masomo yenu”, alisema. Bi Shani alitoa shukurani zake kwa familia za wenyeji na kuwaomba kuendelea na ushirikiano wao na SUZA huku akiwaahidi kuwa mambo mazuri yatakuja.

Kwa upande wake, kiongozi wa wanafunzi hao ambaye ni Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Oregon, Dkt. Mokaya Bosire, kwa niaba ya Chuo chake alianza kwa kuishukuru SUZA kwa uendeshaji mzuri wa kozi kwa wanafunzi wao. Pia nae alitoa shukurani kwa familia wenyeji wa wanafunzi kwa kuishi vizuri na wanafunzi wao.

Alisema wanapendelea Zanzibar kwa sababu hapa ndio wanapata uhalisia wa lugha ya Kiswahili kulinganisha na maeneo mengi yenye wazungumzaji wa lugha hii. Aliendelea kueleza kuwa alifurahia hali ya amani na utulivu iliyopo Zanzibar, hali ambayo imewawezesha wanafunzi wao kusoma kwa utulivu. Aidha alisema kuwa alipenda mazingira yote

ya ndani na nje ya darasa huku akiahidi kuwaletena wanafunzi ili kuendeleza walipoishia kwenye programu hii ya Kiswahili.

Walipopewa nafasi ya kuzungumza kwa niaba ya wahitimu wenzao, wahitimu wawili walisema wanaipenda Zanzibar na walitamani wabaki muda mrefu zaidi. Waliendelea kusema kuwa walifurahia mandhari na ukarimu wa watu wa Zanzibar ambapo ndani ya muda mfupi wa takribani miezi miwili waliyoishi hapa walipata marafiki wengi.

Katika sherehe hiyo, familia za wanafunzi na marafiki wengine walikuja kushereheka na wahitimu na kuwatakiwa kila la kheri. Katika kipindi cha mwaka huu kuanzia Januari hadi Agosti 5, Idara ya Kiswahili kwa Wageni ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ilipokea wanafunzi 70 wanaotoka katika mataifa ya Marekani, Ufaransa, Uingereza, Ubelgiji, Korea Kusini na Ujerumani.

Mataifa mengine ni Uswisi, Poland, Norway, Finland, Itali na Mauritania. Baadhi ya wanafunzi wa mataifa haya wametokea katika Vyuo Vikuu vya Oregon cha Marekani, Chuo Kikuu cha SOAS cha Uingereza, Chuo Kikuu cha Napoli cha Italy, Chuo Kikuu cha Norway pamoja na wanafunzi wanaoletwa kupitia Program ya Foreign Language and Area Studies (FLAS) kutoka Marekani.

Vile vile Idara ilipokea washiriki kutoka Ubalozzi wa Ufaransa na Ujerumani ambao walijiunga kwa kozi ya wiki mbili ya Kiswahili.

Baadae mwezi Agosti SUZA itapokea wanafunzi 12 kutoka Chuo Kikuu cha Humboldt cha Ujerumani ambapo mwezi Septemba wanafunzi wengine kutoka SOAS wanatarajiwa kufika Chuoni kwa masomo ya lugha ya Kiswahili.



SUZA, Turku vyatiliana saini kukuza uhusiano

Na Mwandishi Wetu, SUZA

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Chuo Kikuu cha Turku vimetiliana saini mkataba wa ushirikiano na uhusiano katika masuala ya kielimu na kitaaluma.

Mkataba huo unalenga kuimarisha kuwajengea uwezo wanafunzi na wafanyakazi wa SUZA kiteknolojia, udhamini wa masomo kwa ngazi za juu, ubadilishanaji wa wataalamu kwenye ziara za kimasomo, kupatiwa mafunzo ya ndani katika fani mbalimbali zikiwemo za ujasiriamali, ubunifu na kufanya tafiti.

Akizungumza katika majadiliano mara baada ya kutiliana saini mkataba huo huko Makao Makuu ya SUZA Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja. Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji, alilitaja eneo muhimu la ushirikiano kuwa ni masuala ya uchumi wa buluu ambapo Zanzibar inajiandaa kutengeneza miundombinu ya kuwezesha kutoa taaluma hiyo.

Alisema kuwa tayari ujenzi wa kituo cha kutoa mafunzo hayo umeanza. “Novia wana uzoefu wa masuala ya bahari kwa zaidi ya miaka 200 na kwamba tumeshawishika sana kushirikiana nao”, alisema Prof. Aidha, kwa upande wa kuwajengea uwezo vijana alisema mradi huo utaweza kuwasaidia vijana kujajiri na kuajiriwa. Makubaliano haya

yatawezesha kutumia rasilimali za kielimu na kitaaluma kwa pamoja. Naye Rais wa Chuo Kikuu cha Turku, Jukka Kola ambaye aliongoza ujumbe wa vyuo vikuu vya Finland vinavyoshiriki utekelezaji wa mradi huu, alisema uchumi wa buluu ni eneo muhimu ambapo wataangalia namna bora ya kushirikiana katika eneo hilo.

Aliongeza kuwa kwa vile chuo kina programu za kufundisha masuala yanayohusiana na habari na mawasiliano watazingatia suala hilo pia.

Mradi huu unaodhaminiwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Finland, unatekelezwa kwa pamoja na vyuo vya SUZA, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Ardhi University, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo

Kikuu cha Ushirika Moshi na mashirika ya biashara. Kwa upande wa Finland, vyuo vinavyoshirikiana na Tanzania ni vyuo vikuu vya Turku, Novia na TUAS.

Chuo Kikuu cha Turku (UTU) ni Chuo Kikuu cha umma cha taaluma nyingi kilichopo katika mji wa Turku, kusini magharibi mwa Finland. Ina vitivo vinane na ni moja ya vyuo vikuu vya kimataifa nchini Finland chenye wanafunzi na wafanyakazi kutoka nchi zaidi ya 100.

UTU imeorodheshwa katika orodha ya vyuo vikuu bora ulimwenguni. Chuo kinazingatia utafiti endelevu, elimu, na ushirikiano kwa lengo la kushughulikia masuala mazito ya kisayansi na ya kijamii.

KAMATI YA JARIDA

Mwenyekiti	Ndg. Hassan Simba Hassan
Mratibu	Ndg. Khadija Sadiq Mahumba
Mhariri wa Makala	Dkt. Masoud Nassor Mohammed
Mhariri wa Habari	Dkt. Rashid Maalim Khamis
Mtayarishaji Habari	Ndg. Nasima Haji Chum
Mpiga Mpicha	Ndg. Hamza Makame Ussi
Msanifu Jarida	Ndg. Zedi Abdalla Khamis

Picha za matukio mbalimbali katika sherehe ya uzinduzi wa Kigoda cha Taaluma cha Sheikh Abeid Amani Karume cha Ukombozi na Maendeleo ya Afrika hapo tarehe 15 Juni, 2024 katika Kampasi ya Tunguu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)



Photos that depict various events at the launching ceremony of Sheikh Abeid Amani Karume Professorial Chair of Liberation and Development of Africa on 15th June, 2024 at the Tunguu Campus of the State University of Zanzibar (SUZA)





SUZA, Turku University Sign Agreement to Strengthen Relations

By SUZA Reporter

The State University of Zanzibar (SUZA) and the University of Turku have signed a cooperation agreement to enhance educational and academic relations. The pact aims to build the technological capacity of SUZA students and staff, offer scholarships for advanced studies, facilitate expert exchanges through academic visits, and provide in-house training in various fields, including entrepreneurship, innovation, and research.

Speaking at the signing ceremony held at SUZA's headquarters in Tunguu, South Unguja, SUZA Vice Chancellor, Professor Moh'd Makame Haji, highlighted the key area of cooperation as the blue economy.

He noted that Zanzibar is gearing up to develop the infrastructure necessary to support education in this field.

"The construction of a training center has already commenced, and we have partnered with Novia University to ensure the success of this initiative," said Professor Haji.

"Novia has over 200 years of experience in maritime affairs, and we are highly motivated to collaborate with them."

He added that the project

would empower young people by providing opportunities for self-employment and formal employment, leveraging shared educational and academic resources.

President of the University of Turku, Jukka Kola, who led the delegation of Finnish universities participating in this project, emphasized the importance of the blue economy and the ways they plan to collaborate in this area. "In addition to the blue economy, our university offers programs related to information and communication, which will also be a focus of our cooperation," said Kola. Funded by the Finnish Ministry of Foreign Affairs, this project involves SUZA, Sokoine University of Agriculture, Ardhi University, the

University of Dar es Salaam, Moshi Co-operative University, and business organizations.

On the Finnish side, partner universities include the University of Turku, Novia University, and Turku University of Applied Sciences (TUAS). The University of Turku (UTU) is a multidisciplinary public university located in Turku, southwest Finland. It boasts eight faculties and is one of Finland's most international universities, with students and staff from over 100 different countries.

UTU is ranked among the world's top universities, particularly in sustainable research, education, and collaboration, addressing significant scientific and social issues.

Newsletter Editorial Committee

Chairperson	Mr. Hassan Simba Hassan
Coordinator	Ms. Khadija Sadiq Mahumba
Articles Editor	Dr. Masoud Nassor Mohammed
News Editor	Dr. Rashid Maalim Khamis
News Producer	Ms. Nasima Haji Chum
Photographer	Mr. Hamza Makame Ussi
Newsletter Graphic Designer	Mr. Zedi Abdalla Khamis



SUZA holds graduation ceremony for Oregon Students

By SUZA Reporter

The Department of Kiswahili for Foreigners of the State University of Zanzibar (SUZA) on August 8, 2024 held a graduation ceremony for students from the University of Oregon, USA who graduated their Kiswahili language studies at Vuga Campus. The ceremony celebrated the achievements of 8 students who successfully completed a seven-week programme of elementary and advanced levels.

Dr. Abubakar Makame Fakihi, the Dean of the School of Kiswahili and Foreign Languages, who graced the graduation occasion on behalf of the Vice-Chancellor, praised the efforts of the graduates for completing their Kiswahili language and its cultural studies successfully.

He also said the short time they spent here in SUZA has been able to create an experience that is no longer easy to disappear. He further expressed that the progress they had made needed to be developed, so he urged them in another stage of the advancement of Kiswahili language studies to return to SUZA to develop this language profession which is now an internationally recognized.

The School Dean also did not disregard thanking the host families for staying with students living with them in worthy life in their houses keeping with the authentic Kiswahili traditions. He urged the students to be good ambassadors in promoting SUZA, Zanzibar and Tanzania as a whole, and to express the hospitality and tranquillity prevailing in Zanzibar.

He wished the students to travel and reach their destinations safely. "I wish you great success and happiness in the years to come," he told them.

Earlier, the Head of the Department of Kiswahili for Foreigners, Ms. Shani Suleiman Khalfan expressed gratitude to all those who participated in the ceremony.

Ms. Shani told the graduates that there is nothing more difficult in life than saying goodbye to the person or people you have been paired with. "We would like to be with you all the time, but the situation does not allow it", she informed.

"Today doesn't mark the end of your relationship with us here at the Department. After this graduation, you will join us as members of the Department of Kiswahili for Foreigners' alumni community, with over hundreds of people all over the world", she said.

"We hope that you will continue learning the language and culture of Kiswahili in the course of your studies," she explained. Ms. Shani expressed her gratitude to the host families and asked them to continue with their cooperation with SUZA while promising them that good things are to come.

On his side, the students' supervisor, who is the lecturer of the University of Oregon, Dr. Mokaya Bosire on behalf of his university, began by thanking SUZA for the excellent conduct of the course for their students. He also thanked the host families for living well with their students.

He said they prefer Zanzibar because this is the place where they get the authenticity of Kiswahili language compared to many places with speakers of this language.

He went on to explain that he enjoyed the peaceful and quiet atmosphere in Zanzibar, which has enabled their students to study in composure. He also said he was pleased by the environment both

inside and outside the classrooms, and promised to bring students back to continue with where they ended up in their programme. When given the opportunity to speak on behalf of their fellow graduates, two graduates said they loved Zanzibar and wished they could stay longer. They went on to say that they enjoyed the scenery and hospitality of the people of Zanzibar where within a short time of nearly two months they lived here they made many friends.

On the ceremony, students' host families and some friends came to celebrate the success of the graduates and expressed their best wishes to them.

In this year from January to August 5, the Department of Kiswahili for Foreigners of the State University of Zanzibar received 70 students from the United States, France, Britain, Belgium, South Korea and Germany

Other nations are Switzerland, Poland, Norway, Finland, Italy and Mauritania. Some of the students from these nations have come from the University of Oregon of the United States, the School of Oriental and African Studies (SOAS) of the United Kingdom, the University of Naples of Italy, the University of Norway as well as the students brought through the Foreign Languages and Area Studies (FLAS) Program from the United States.

The Department also received participants from the French and German Embassies who joined for the two-week Kiswahili course.

Later in August SUZA will receive 12 students from Humboldt University of Germany, while in September the other students from SOAS are expected to arrive at the University for Kiswahili language studies.



Lela praises Universities for Introducing Confucius Class

By SUZA Reporter

The Minister of Education and Vocational training Hon. Lela Muhammed Mussa praised the State University of Zanzibar (SUZA) and Zhejiang Normal University (ZJNU) for their strong support to the formation of the Confucius Class. Speaking at the inaugural ceremony of Zanzibar Confucius class at Maruhubi SUZA campus, Hon. Lela said the setup of the language learning programme in Zanzibar is a symbol of close ties between the duo and a symbol of friendship and cooperation that has existed for a long time. Hon. Lela said that the Confucius Class at SUZA offers Chinese language skills for Diploma and Degree students of SUZA and two other educational institutions which are Zanzibar University and Leera school which have joined the programme this year. "I am very optimistic that the programme will reinforce a historic relationship between Zanzibar and China", she said. She further added that Chinese language has become prominent worldwide and incorporated in the national education system in 85 countries whereas more than 1,300 Chinese language proficiency testing centres have been established in 160 countries. However, she called upon SUZA management to encourage more schools to join Confucius team hence intensify ties between China and Zanzibar. The Vice-Chancellor of SUZA Prof. Moh'd Makame Haji asked fellow government officials, members of business community and young men and women to learn Chinese language and culture so as to enable them fully adapt it. "I request all entrepreneurs of Zanzibar to come and join the Confucius Class and be part of the pioneer beneficiaries

of what SUZA offers", he insisted. Citing on the relationship, the Vice-Chancellor commented that the brotherly bilateral relationship between China and Tanzania have withstood with the change of international situation and grown closer than ever. "Under the guidance of the Forum on China-Africa Cooperation and its action plans, the friendly cooperation between China and Tanzania has made a great stride and written a new chapter featuring political equality and mutual trust, a win-win economic

and cultural exchange," he said. Addressing the meeting, the Chair of the ZJNU Council Prof. Jiang Yunliang appreciated the SUZA management team for their support toward the establishment of the Confucius Class.

He further said that the programme will be an instrument to provide an opportunity of understanding culture and promoting mutual benefits from this partnership between our nations.

New outlook in pipeline at SUZA Main Campus

By SUZA Reporter

The Vice-Chancellor of the State University of Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji, said the University is in the process of its infrastructure transformation by developing a major reform plan for SUZA's expansion of the next 20 years.

Talking in a staff meeting at Tunguu campus Prof. Haji informed that the plan would intensify the strength of working and go hand in hand with change and raising the hopes of the country's senior leaders to see institutions work effectively and are beneficial at this time and in the future.

He mentioned the projects that are expected to bring about major reforms to be Higher Education for Economic Transformation (HEET) project, which will construct modern buildings including a large modern laboratory, hostels for male and female students and the buildings for School of Agriculture. He noted that another project funded by the Arab Bank for African Development (BADEA) in which the Revolutionary Government of Zanzibar is investing 10% of the project to construct a range of buildings including sports fields.


"Since SUZA is involved in the sports industry, the it will construct Olympic-level sports fields and staff residential houses", he said.

The Vice-Chancellor went on to inform that there will be modern venues offering a variety of amenities such as parking, food service access points and supermarkets which will also be rented out.

"By the time we finish we will have erected 39 buildings where all the schools under SUZA and others that have not been established but are under envisaged plan will also be built," he explained.

He encouraged stakeholders to be cooperative to the maximum for everyone to be part of SUZA for the sake of giving direction to where the institution wants to go. We want to create a good university which is in line with its vision and mission, he added.

Last year, SUZA ranked among the best universities in Africa selected for the quality of work it does by ranking 157th out of 200 university despite its age as compared to other universities. "This is not a minor position compared to the 1,274 universities in Africa," the Vice-Chancellor informed.



SUZA, HNU Strengthen Collaboration

By SUZA Reporter

A delegation from China's Hunan University (HNU), led by Vice President Dr. Wang Weibin, recently paid an official visit to the State University of Zanzibar (SUZA) to strengthen collaborative opportunities between the two institutions.

This partnership aims to prioritize various areas related to teaching, research, and consultancy, with plans to expand cooperation across many other areas. Contributing to the discussions, SUZA Vice-Chancellor Prof. Moh'd Makame Haji expressed his satisfaction with the newly established relationship, which is expected to bring significant changes and development.

"I believe our collaboration can be mutually beneficial, enhancing educational opportunities for our students and contributing to community development," he added. Prof. Haji mentioned that, despite the increasing number of youth seeking employment, SUZA has been empowering them by providing them with skills in various areas, including entrepreneurship.

He believes that this partnership will be beneficial for both institutions by enhancing skills, expertise, and community development. On his part, Hunan University Vice-President Dr. Wang Weibin emphasized that communication is crucial for HNU and SUZA as it can facilitate knowledge exchange, experience sharing, and cultural learning between the two sides. Dr. Wang noted that

Tanzanian students have been enrolled at HNU since 2014, and the collaboration continues to promote joint research initiatives between Chinese and Tanzanian academics.

"HNU educates many students in various fields. I hope our partnership will be even more fruitful, especially in continuing our efforts in Tanzania, particularly in Zanzibar," he said. Discussing the Institute of African Economics, Business, and Research, Dr. Wang revealed that the institute was established to foster close communication

and good relationships with other African universities. Hunan University (HNU) is located in Changsha, the capital of Hunan Province in China, a city renowned for its history and culture, situated near the Xiangjiang River and Mount Yuelu. Founded in 976 AD, Hunan University is one of China's oldest higher education institutions, continuously promoting cultural education and serving as a model for the advancement of higher education in China.

Kiswahili becomes World's best Commodity

By SUZA Reporter

The Vice-Chancellor of the State University of Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji, stated that the Kiswahili language has become a premium commodity worldwide due to its significance which led to be taught in various universities, used in media broadcastings and in business.

Prof. Haji made these remarks during a conversation with the French and German ambassadors, who visited the country for a two-week tour aimed at learning about Zanzibar's history and the participation of women in decision-making levels in Tanzania.

He informed the delegation about the efforts of different countries to strengthen Kiswahili within their borders and he stated that universities from Nigeria and South Africa recently visited Zanzibar seeking advice on how to enhance the language in their countries, including curriculum development.

"China has universities and media outlets using this language, and even Zanzibari traders speak it," the Vice-Chancellor said. Prof. Haji added that there are many opportunities economically and commercially, consequently SUZA needs to help widening these

opportunities through emphasizing it by applying ICT in order to reach a wider audience in the world. Discussing on the history of Kiswahili language in Tanzania, Prof. Haji clarified that if there is an issue that the Father of Nation triumphed in, is making Kiswahili language to become the national language among more than 125 tribal languages found in Tanzania.

The Vice-Chancellor noted that while this language is being recognized as an official language in African Union countries, Kiswahili is also spoken in nearly all African nations. "Kiswahili is different from other languages like Yoruba, which, despite having many speakers, is only spoken within a single region in Nigeria," he stated. Earlier, the Acting Head of the Kiswahili for Foreigners Department, Ms. Ziada Tajo Ameir, stated that the eight-person delegation learned Kiswahili in the context of politics and Islamic religion, the Zanzibar political ruling before and after the 1964 Revolution up to the era of multiparty leadership.

Other areas of learning included human rights and the roles of women in leadership within the Zanzibar House of Representatives and the Parliament of the United Republic of Tanzania.



SUZA Sets Plans in Motion to Launch Marine Science Studies

By SUZA Reporter

In a significant move towards enhancing marine education, the Vice-Chancellor of the State University of Zanzibar (SUZA), Prof. Mo'hd Makame Haji, convened a meeting with marine experts to deliberate on the initial steps for establishing a Marine Studies Institute.

During the discussions held at the Vice-Chancellor's office in Tunguu, Prof. Haji highlighted the progress SUZA has made in setting up the institute, which aims to provide comprehensive marine training. He emphasized that the Revolutionary Government of Zanzibar is fully supportive of this initiative.

Prof. Haji elaborated on SUZA's ongoing collaboration with the Ministry of Education and Vocational Training and other stakeholders involved in marine and Blue Economy matters. "We aim to develop essential talents, including engineers, diving specialists, meteorologists, and other professionals in fields related to the Blue Economy, meeting international standards," he asserted.

"Our goal is to empower individuals through specialized programs, equipping them with skills to achieve the economic production targets set by our government," he added. Prof. Haji expressed opti-

mism that significant success would be realized through SUZA's partnership with other stakeholders.

Dr. Yahya Sheikh, Head of the Department of Marine Science at SUZA, presented the framework for establishing the Marine Training Commission. He announced that eight students are expected to receive overseas training in marine studies.

"To produce top-notch practitioners, learning from other experts in their field is crucial. We anticipate their contributions in developing the institute's curriculum," he stated.

Dr. Sheikh added that the institute plans to start marine studies with an initial intake of one thousand students and has aspirations to establish another training center in Pemba.

He mentioned that these programs are expected to boost the seaweed trade in Pemba, where the cultivation thrives.

"These initiatives will greatly benefit the Revolutionary Government of Zanzibar. Addressing Blue Economy issues without such training are problematic," he noted. Representatives from the Maritime Capacity Alliance, including Commander Pepijin Verstand and his colleague Ericjan de Roode from

the Netherlands, expressed their satisfaction with SUZA's steps towards establishing the Marine Studies Institute. Commander Verstand provided insights into setting up an initial training institute for commanders in the country by June, emphasizing the need for a phased approach.

"We expect Tanzania to become a major player in marine affairs. By adhering to international laws and standards, we can bring in instructors to train the locals," Commander Verstand said.

He also underscored the importance of maritime safety, which can enhance tourist security, combat smuggling, and track all vessels passing through the region.

The meeting between SUZA officials and the Maritime Capacity Alliance included discussions on various aspects of marine training, such as port and vessel security, mariner discipline, curriculum development in collaboration with other marine institutions, preparation of local instructors, and establishing student entry standards.

The necessity of a Communication Strategy was also highlighted, focusing on involving the community and fishermen.



Timely Accountability Mitigates Challenges - PAC

By SUZA Reporter

The Public Accounts Committee (PAC) of the Zanzibar House of Representatives has urged the State University of Zanzibar (SUZA) to promptly implement the recommendations provided by the Controller and Auditor General (CAG) to prevent potential challenges. The advice was issued during discussions between the PAC and SUZA regarding the 2021/2022 financial and IT system audit report at SUZA's headquarters in Tunguu, South Unguja District.

The committee emphasized that they have advised SUZA on numerous issues aimed at improving the efficiency of its operations, highlighting that swift action on these recommendations would yield quick success.

“Taking timely action will reduce potential negative impacts. When the CAG provides advice, it should be acted upon professionally and swiftly to achieve success,” stated Hon. Mohammed Abdallah Salum, a member of PAC.

Earlier, the Vice-Chancellor of SUZA, Professor Moh'd Makame Haji, admitted to delays in the university's fiber optic connection due to some campus-

es not being established at the time of the system integration.

“The operation of the system has faced many challenges, and educational institutions need an optimal system, which has now been addressed. The fiber optic connection has been completed, and system services are functioning normally,” said the professor.

Responding to questions about the university's budget and operations, Professor Haji confirmed that everything is progressing well. He stated that the university has cleared all debts from 2014 to 2024, with remaining debts pertaining to ongoing contracts, such as the construction of buildings at Mbweni and Dakhalia campuses in Chwaka.

Engineer Robert Mwelo, a government systems auditor, acknowledged that SUZA has a large community of students and staff, including accountants who need this crucial service to perform their duties. Additionally, he emphasized the importance of prioritizing the IT systems budget to address the challenges of network service availability.

“Without this service, students cannot learn, and accountants will be unable to perform their tasks on time,” he reminded.

The Chairman of the committee, Hon. Juma Ali Khatib, expressed satisfaction with SUZA's performance in efficiently responding to all issues raised by the CAG.

